**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA**

**Shule ya Sekondari Kiomoni**
**S.L.P 2369 Tanga**
**Tarehe ................**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WAVULANA KIOMONI, HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA MKOA TANGA MWAKA………………**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka…..……..…na atasoma Tahasusi ya **………..** Aidha, ninampongeza sana mwanao kuwa miongoni mwa vijana wachache waliopata nafasi ya kujiunga na kidato cha Tano katika Shule za Serikali.

Shule ya Sekondari ya Wavulana Kiomoni ni Shule ya Bweni na ipo Kata ya Mzizima, mtaa wa mafuriko umbali wa takriban Kilometa **14** kaskazini mwa Jiji la TANGA.
Usafiri wa basi/Daladala muda wote unapatikana. Kwa wanaotoka Mikoani, kutokea kituo kikuu cha mabasi **KANGE** panda daladala zinazoenda Stendi ya zamani. Ukifika stendi ya zamani, panda daladala zinazoenda Amboni/Mabokweni kupitia barabara ya Tanga - Horohoro. Shuka Kituo cha Mafuriko. Kutoka kituo cha Mafuriko nauli ni Shilingi **1,500** kwa pikipiki na Shilingi **4,000** kwa bajaji kupitia barabara ya kuelekea Kihongwe.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe…………….., hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni Tarehe………………Mwisho wa kuripoti ni Tarehe …./…/……......

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1. Sare za Shule

i. Mwanafunzi aje na za Sare ya Shule ambayo ni suruali mbili za rangi ya **kijivu** (isiwe Modo) au kama Mzazi itampendeza Sare hizo zinapatikana Shuleni kupitia fundi aliyepo kwa gharama ya Tsh **18,000** kwa kila moja.
ii. Awe na Mashati mawili ya tetroni, meupe ya mikono mifupi na **tai ndogo** shingoni
iii. Aje na Sare ya Michezo ni **trak suti** moja na **bukta** moja rangi ya blue bahari (light blue)
iv. Aje na Viatu vya Shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi. Visiwe buti
v. Awe na Soksi jozi mbili nyeupe za Shule;
vi. Aje na Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
vii. Awe na Sweta rangi ya **brown** mikono mirefu lenye shingo ya V (**v-shaped**) au kama mzazi itampendeza Sweta hiyo inapatikana shuleni kwa bei ya shilingi **15,000/=**
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) ni suruali moja (nyeusi) na Tisheti (Nyeupe). Aje akiwa amezivaa siku ya kuripoti. **Nguo za nyumbani haziruhusiwi**.
ix. Aje na Tisheti (T-shirt) ya kola rangi ya **brown,** kama mzazi itampendeza T-shirt hiyo inapatikana Shuleni kwa bei ya shilingi **13,000/=**
x. Kila mwanafunzi anatakiwa Kuweka alama kwenye nguo na vifaa vyake atakavyokua navyo hapa Shuleni au kama itampendeza Shule inaweka alama kwenye nguo na vifaa vyote vya mwanafunzi kwa gharama ya Tsh **10,000/=**

## 3.Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Aje na Madaftari **12** ya counterbook (quare 3) Aje na **Ream Mbili (A4)** za Karatasi nyeupe kwa mwaka. Mzazi ukipenda Rimu zinapatika jirani na Shule kwa bei ya Tsh. **14,000/=**
ii. Aje na **Rimu rulled Mbili (A4)** za Karatasi za Mistari kwa mwaka,kwa ajili ya kujibia Mitihani ya ndani Shuleni. Mzazi ukipenda *Rulled paper* zinapatika jirani na Shule kwa bei ya Tsh **11,000/=**
iii. Aje na Vitabu vya masomo ya Tahasusi husika.
iv. Aje na Begi jeusi la kubebea madaftari.Mabegi ya aina nyingine hayaruhusiwi
v. Aje na Sanduku la bati (**tranker** ) lisilozidi urefu wa mita moja
vi. Aje na **Dissecting Kit na stop** watch kwa wanafunzi wa Tahasusi ya **PCB**
vii. Aje na Scientific Calculator kwa wanafunzi wa Tahasusi ya **PCB** na **EGM**, Aidha wote waje na tochi, kwa matumizi yake binafsi
viii. Aje na Godoro **jipya** kwa wanafunzi lenye urefu futi **6**, upana futi **2.5** na unene inchi **6**

ix. Mwanafunzi anatakiwa aje na Mashuka ya rangi ya **pink Jozi 2** au mzazi ikikupendeza Mashuka yanapatikana Shuleni kwa gharama ya Tsh 8,000/= kwa kila Moja
x. Aje na Mto na Foronya **2** za **Pink**, chandarua kimoja cha rangi ya **blue** au mzazi ikikupendeza vinapatikana Shuleni kwa bei nafuu.
xi. Aje na Nguo za ndani za kotoni za kutosha
xii. Aje na Taulo la Kotoni na ndala pea 1 za kuogea
xiii. Aje na Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe )
xiv. Aje na Ndoo 2 ndogo (Za lita Kumi) zenye mifuniko;
xv. Kwa wanafunzi wa mchepuo wa PCB waje na Kwanja 1 na fagio 1 gumu la dukani (Hard broom). Kwa wanafunzi wa mchepuo wa EGM waje na squiza moja na fagio 1 laini la dukani (Soft broom), kwa mchepuo wa HGL waje na Mopper moja na kindoo chake.
N.B. Kwa mzazi atakayependa, Ndoo, Kwanja, Hard broom, Soft broom Squiza na Mopper vinapatikana Shuleni kwa bei nafuu;
xvi. Unatakiwa uje na kopo lako la kuogea
xvii. Mwanafunzi aje na cheti cha matokeo ya kidato cha nne (Result slip) wa mwaka aliomaliza
xviii. Mwanafunzi aje na nakala ya cheti chake cha kuzaliwa.

**4. Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Michango hii tu ndiyo iwekwe kwenye akaunt ya Shule **namba 41701200075 NMB jina la akaunti - Kiomoni Secondary School. Mwanafunzi aje na Original *Pay in Slip* ya benki siku ya kuripoti Shuleni**

## 4.. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya utungaji wa Sera za elimu nchini pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na Mwanafunzi utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti Shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 4.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya Shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku ( Preparation )
iv. Kuwahi katika kila shughuli za Shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika Shule hii;
vi. Kutunza usafi wako wa mwili, mavazi na mazingira ya Shule;
vii. Kuvaa sare ya Shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za Shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo Shuleni.
xii. Kufeli, kutofanya mitihani au kupata alama “F” kwenye mitihani ya somo lolote na mazoezi darasani ni kosa lisilovumilika, ikitokea hivyo utagharamia Mitihani hiyo mwenyewe.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu Shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi akikamatwa na simu hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.**
- **Mwanafunzi awapo Shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi**

**kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (i.e Msiba au Ugonjwa**).

### 4.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku **90** bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha migomo Shuleni;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu mwingine yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo wowote ule;
vii. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo Shuleni;
viii. Kufuga ndevu;
ix. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
x. Uvutaji wa sigara;
xi. Uasherati, mahusiano ya jinsia moja, kuoa au kuolewa;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu;
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi; na
xviii. Kumiliki, kukutwa au kutumia **simu** ya mkononi katika mazingira ya Shule

## 5. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya ( Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga wa Hospitali ya Serikali inayotambulika.
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na Shule na
iv. Picha nne (**4**) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi Shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA SHULENI KIOMONI SS**

…………………

**KAANA ERASTO**
**MKUU WA SHULE**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. Tafadhali upatapo ujumbe wowote kuhusu mwanafunzi/mtoto wako usitume chochote, ni vema ukawasiliana na uongozi wa Shule kupata ukweli wa taarifa husika kwa namba zifuatazo: -**

- **Mkuu wa Shule 0784832358 Au 0656047861**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0653144068 Au 0719504686**
- **Mwandamizi Taaluma 0717616343**
- **Mwandamizi Malezi 0715577115**

**OFISI YA WAZIRI MKUU,TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI KIOMONI**
**S.L.P 2369**
**TANGA**

---

## FOMU RASMI YA KUANDIKISHWA

**PICHA YA MWANAFUNZI**

**SEHEMU A IJAZWE NA MWANAFUNZI**

1. Jina la mwanafunzi……………………………………………………………2. Uraia……………………………
3. Dini…………………………………………….4. Tarehe ya kuzaliwa ………………………...............
5.Shule uliyosoma kabla ya kuja Kiomoni Sekondari…………………………………………
Sahihi ya mwanafunzi ……………………………………………………………Tarehe……………………..

**Picha ya Mzazi/Mlezi**

**SEHEMU B: MAELEZO BINAFSI YA MZAZI /MLEZI**

1.Jina kamili …………………………………………………………2. Anuani…………………………………………
3.Wazazi wapo Hai /Wamefariki Baba /Mama. Mtoto Anaishi na ………………………………
4.Wilaya ………………………………… Tarafa……………………………………..Kata…………………………
Mtaa ……………………………………..Jina la M/kiti wa Mtaa …………………………………………
Anuani ya Mwenyekiti wa mtaa…………………………………..........................................

4. Kazi unayofanya ……………………………………5. Namba ya simu :Baba/Mama……………………………

**SEHEMU C; KUKIRI**

Mimi ………………………………………..mzazi /mlezi wa …………………………………………Nimesoma vyema sheria kanuni na taratibu za Shule. Nakubali /Sikubali mwanangu ajiunge na Shule ya Sekondari Kiomoni. Nitahakikisha kuwa mwanangu anapata mahitaji yote muhimu ya Shule na kufuatilia kwa ukaribu maendeleo yake ya kitaaluma na nidhamu Shuleni. Iwapo mwanangu atakwenda kinyume na sheria /taratibu za Shule nakubali awajibishwe ipasavyo. Nitakuwa tayari muda wote kuitikia wito wa walimu na nitakuwa nikihudhuria vikao mimi mwenyewe.
Sahihi ya Mzazi /Mlezi……………………………Tarehe ……………………………

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi ……………………………………………………………nakubali /sikubali nafasi niliyopewa katika Shule ya Sekondari Kiomoni.
Naahidi kuwa nitazitii kanuni na sheria zote za Shule. Nitafuata masharti yote yatakayotolewa na Mkuu wa Shule, Walimu na viongozi wote wa Shule .

Naahidi pia kuwa nitashirikiana na wanafunzi wenzangu katika shughuli za masomo, kazi za nje na katika michezo ili kuinua kiwango cha Taaluma, mazingira safi na kukuza jina zuri la Shule yetu ya KIomoni.

**……………………**
**Saini ya mwanafunzi**

**Tarehe …………………………….**

**GOVERNMENT OF TANZANIA**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

KIOMONI SEC. SCHOOL
P.O BOX 2369
**TANGA**

TO: MEDICAL OFFICER
…………………………………
…………………………………

**RE: MR/MISS (Full Name) ……………………………………………………………………………………………….**
Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full-time schooling course. The examination should include the following categories (i–iii) each category or subcategory of which will render the applicant ineligible in case of a defect. (a) Eye – sight.
(b) Hearing
(c ) Limbs
(d) Speech
(e) Venereal Diseases (s)
(f) Leprosy
(g) Epilepsy
**(ii)** Neurosis
**(iii)** Other serious diseases

**Signature ………………………………………………….**

---

**PART B**
**MEDICAL CERTIFICATE**
**(**To be completed by Medical officer )
I have examine the above named and consider that he is physically fit/ unfit and mentally fit/ unfit for a full a time schooling course.
**i**. (a) Eye - sight …………………………………(b) Hearing ……………………………………..
(c ) Limbs ……………………………………………(d) Speech………………………………………
(e) Veneral Diseases ……………………………(f) Leprosy ……………………………………
(g) Epilepsy…………………………………………
**ii**. Neurosis…………………………………………………..
**iii**. Other serious diseases………………………………………..

Signature………………………………………..
Station …………………………………………..  Designation…………………………………..
Date……………………………………………